Makala Maalum

MFUKO WA UADILIFU, UWAJIBIKAJI NA UWAZI NI MSHIRIKA MUHIMU KATIKA KUIMARISHA UTAWALA BORA NCHINI.

Jitihada za serikali za kuimarisha misingi ya utawala bora nchini zinazidi kupata nguvu kutoka kwa wadau mbalimbali hususani washirika wa kimaendeleo wa kimataifa (Development Patners). Tarehe 5 Juni 2006, Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa (IDA) zilikamilisha makubaliano
ya utekelezaji wa mpango wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi na hatimaye kuanzishwa kwa Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi.

Makala haya yanalenga kuonyesha umuhimu wa Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi katika kuimarisha Utawala Bora nchini.

Kwa kuanzia Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi ni Mfuko wa kusaidia Taasisi na Asasi zenye kujihusisha na masuala ya Utawala Bora ili ziweze kutekeleza na kufuatilia shughuli za kuboresha na kuimarisha Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi kwa lengo la kudumisha Utawala Bora nchini. Mfuko huu ulizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dr. Ali Mohamed Shein, tarehe 26 Septemba 2007.

Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi umejikita zaidi katika suala la Utawala Bora kutokana na ukweli kuwa Utawala Bora ni nguzo muhimu katika kuchochea jitihada za wananchi za kujiletea maendeleo. Aidha, katika taarifa yake kwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa Mfuko huo, Kamishna wa Maadili ambaye pia ni Mwenyekiti wa Mfuko huu Mh. Jaji Mstaafu Stephen Ihema alimnukuu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Jakaya Kikwete ambaye aliwahi kusema katika moja ya hotuba zake kuwa "Serikali inayoendeshwa kwa misingi ya Utawala Bora inazo sifa kubwa ambazo ni pamoja na Uwazi na Uwajibikaji." Hii ni kutokana na ukweli kuwa uwajibikaji na uwazi wa viongozi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao inaongeza imani ya wananchi kwa viongozi wao.

Umuhimu wa Utawala Bora unaonekana pia kwenye Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, yaani MKUKUTA. Utawala Bora na Uwajibikaji ni moja wapo ya nguzo kuu tatu za MKUKUTA. Nguzo mbili nyingine ni Ukuaji wa Uchumi na Kupunguza umaskini wa Kipato; na Kuimarisha ubora wa maisha na Ustawi wa Jamii.

Akitoa hotuba yake katika uzinduzi wa Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dr. Ali Mohamed Shein alisema kwamba uzinduzi wa Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi ni hatua ya moja kwa moja ya utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania, yaani MKUKUTA.

Kimsingi Utawala Bora ndio nguzo mama ya MKUKUTA ambayo uimara wake ndio utakaopelekea malengo ya nguzo mbili nyingine ambazo ni Kupunguza Umaskini wa Kipato; na Kuimarisha Ubora wa Maisha na Ustawi wa Jamii kufikiwa. Akifafanua kuhusiana na suala hilo katika uzinduzi huo, Makamu wa Rais Dr. Ali Mohamed Shein alisema kuwa Utawala Bora katika MKUKUTA, ni mhimili wa nguzo hizo nyingine mbili. Alisema:-

“Hii ni nguzo inayotoa wito wa kuwa wazi na kuwajibika, si kwa Serikali tu, bali pia kwa wote wanaohusika kuondoa rushwa nchini Kuhakikisha kuwa, watu wanapata taarifa na habari muhimu, Kuwa na mfumo wa sheria unaozingatia usawa, Kujenga uwezo wa watu; na kuuimarisha uongozi na usimamizi wa asasi, kuanzia ngazi ya wananchi hadi Serikali Kuu”

Ikiwa Taasisi na Asasi zinazojishughulisha na Uwajibikaji, Uadilifu na Uwazi zitautumia vizuri Mfuko huu, utawezesha kupatikana kwa matokeo yanayotarajiwa chini ya nguzo ya MKUKUTA ya utawala na uwajibikaji ambayo ni pamoja na Utawala Bora na Utawala wa Sheria, Uwajibikaji wa Viongozi na watumishi wa umma, Demokrasia na kuvumiliana kisiasa na kijamii na mwisho ni amani, utulivu wa kisiasa, umoja wa kitaifa na mshikamano wa kijamii.

Taasisi na Asasi nyingi nchini zinazojishughulisha na Uwajibikaji, Uadilifu na Uwazi zinakabiliwa na changamoto nyingi katika kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na

kukosa msaada ili kujijengea uwezo wa kutekeleza na kufuatilia shughuli za kuboresha na kuimarisha Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi kwa lengo la kudumisha Utawala Bora nchini. Hivyo kuwepo kwa Mfuko huu utakuwa ni ukombozi mkubwa kwa Taasisi na Asasi hizo kufikia lengo hilo kwa maslahi na ustawi wa jamii ya Tanzania.

Mpaka sasa zipo shughuli kadha wa kadha ambazo zimeshafanyika tangu kuanzishwa kwa Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi. Akisoma risala ya kumkaribisha Mgeni rasmi katika uzinduzi wa Mfuko huo, Kamishna wa Maadili ambaye pia ni Mwenyekiti wa Mfuko huo Mh. Jaji Mstaafu Stephen Ihema alizitaja baadhi ya shughuli zilizofanyika ambazo ni pamoja na kuandaa Mpango Kazi, Mpango wa Bajeti, na Taratibu za Kuendesha Mfuko yaani (Operations and Financial Management Manual for FEAT). Taratibu hizo ni pamoja na Mwongozo wa Kuwasilisha Fomu ya Maombi, Muundo wa Mkataba wa Ruzuku/Ufadhili na Taarifa/Ripoti ya Mwisho wa Mradi uliofadhiliwa.

Aidha, kazi nyingine ambayo imefanyika ni kuutangaza Mfuko kwa wadau kupitia njia mbalimbali, mathalan, katika kipindi cha mwaka 2007/2008, Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi ulichapisha Kalenda zilizobeba ujumbe unaohusu Mfuko ambazo zilitolewa kwa Taasisi za Umma, Binafsi pamoja na wananchi mbalimbali. Katika jitihada hizo hizo, Mfuko umekamilisha kuandaa makala “Documentary” inayoelezea pamoja na mambo

mengine, madhumuni ya uanzishwaji na walengwa wa Mfuko huu ambayo inarushwa kupitia kituo cha Luninga cha TBC1.

Jitihada za kuutangaza Mfuko zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa, kwani katika kipindi kifupi tangu kuzinduliwa na kutangazwa kwa Mfuko huo mwitikio wa Taasisi na Asasi mbalimbali zinazosimamia na kujishughulisha na uwajibikaji, uadilifu na uwazi kuwasilisha maombi ya ruzuku kwa Meneja wa Mfuko wa Uadilifu, Uwajibikaji na Uwazi umekuwa ni mkubwa kuliko ilivyotazamiwa.

Awamu ya kwanza ya kuwasilisha mombi ya ruzuku ilianza mara baada ya uzinduzi wa Mfuko tarehe 29 Septemba 2007 mpaka tarehe 31 Disemba, 2007. Katika kipindi hicho, Mfuko ulipokea jumla ya maombi 177 kutoka kwenye Asasi na Taasisi mbalimbali ambapo Kamati ya Uendeshaji ilikaa na kuyafanyia uchambuzi maombi hayo na hatimaye maombi 11 yalifuzu kupata ruzuku wakati maombi mengine 166 hayakufanikiwa kupata ruzuku kutokana na kasoro mbalimbali zilizobainika na kurudishwa kwa waombaji ili warekebishe kasoro hizo.

Hata hivyo kuna haja ya Taasisi pamoja na Asasi hizo kuzingatia vigezo mbalimbali vilivyowekwa na Mfuko ili kuepuka usumbufu unaoweza kutokea ikiwamo pamoja na kukataliwa kwa maombi yao. Kimsingi lengo la kuwekwa vigezo hivyo sio kuweka ugumu wa kupata ruzuku bali ni kuhakikisha kuwa waombaji wanazingatia taratibu zilizowekwa na Mfuko sambamba na hilo

ni kuendeleza dhana ya uwazi katika matumizi ya fedha za umma.

Awamu ya kwanza ya kuwasilisha maombi ilikamilika tangu tarehe 31 Disemba 2007, lakini Mfuko bado utaendelea kupokea maombi ya ruzuku katika kipindi cha miaka mitatu hadi minne ijayo na taarifa za kuanza kutolewa kwa ruzuku zitakuwa zinatolewa kupitia vyombo vya habari.

Mfuko unapenda kutoa wito kwa Taasisi na Asasi zinazojishughulisha na masuala ya Utawala Bora kuendelea kuwasiliana na Ofisi ya Meneja wa Mfuko katika Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Mtaa wa Ohio Dar es Salaam, au katika Ofisi za Kanda za Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Arusha, Dodoma, Mtwara, Mbeya, Tabora na Mwanza.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:-
Meneja Mradi,
Ofisi ya Rais,
Sekretarieti ya Maadili ya
Viongozi wa Umma,
S.L.P 13341,
Simu: 022 2111810/11
Faksi: 022 2119217
DAR ES SALAAM